

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANI  
WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI  
JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**



**TANGAZO LA NAFASI ZA AJIRA**

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji anatangaza nafasi za ajira kwa vijana waliohitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) na walioko kambini wenye sifa zifuatazo:-

**1. Wenye elimu ya kidato cha Nne (Nafasi 180)**

- (i) Waliohitimu kidato cha nne kuanzia mwaka 2015 hadi 2020.
- (ii) Wenye astashahada, Trade-Test Grade I, FTC na ujuzi katika fani zifuatazo watapewa kipaumbele:-
  - a. Udereva Daraja E
  - b. Ufundi Magari
  - c. Ushonaji
  - d. Ufundi bomba
  - e. Ufundi ujenzi
  - f. Ufundi Umeme
  - g. Uogeleaji/Uzamiaji
  - h. Sayansi ya moto kutoka chuo cha Zimamoto na Uokoaji au chuo kingine kinachotambuliwa na serikali.
  - i. Clinical Assistants
- (iii) Umri kuanzia miaka 18 hadi 23

**2. Wenye elimu ya Kidato cha sita katika michepuo ya sayansi (Nafasi 50)**

- (i) Waliohitimu na kufaulu kidato cha sita kuanzia mwaka 2015 hadi 2020
- (ii) Umri kuanzia miaka 18 hadi 25

### 3. Wenye Shahada au Stashahada ya Juu (Nafasi 20)

- (i) Waliohitimu shahada/stashahada ya juu katika fani zifuatazo:-
  - a. Usanifu Majengo
  - b. Uhandisi wa mawasiliano
  - c. Uhandisi wa Umeme
  - d. Uhandisi wa Majengo
  - e. Uhandisi wa Mitambo
  - f. Uhandisi wa Mafuta na Gesi
  - g. Sheria (aliyesoma na kufaulu shule ya sheria kwa vitendo)
  - h. Ualimu katika somo la Fizikia
  - i. Ualimu katika somo la Kemia
  - j. Ualimu katika somo la Biolojia
- (ii) Umri kuanzia miaka 18 hadi 28.

### 4. Sifa za mwombaji

- (i) Awe raia wa Tanzania kwa kuzaliwa.
- (ii) Awe amehitimu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) au aliyepo kambi ya JKT.
- (iii) Awe na cheti cha kuzaliwa.
- (iv) Awe na Kitambulisho cha Taifa au Namba ya Utambulisho iliyotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho.
- (v) Awe na afya njema ya kimwili na kiakili.
- (vi) Asiwe na Kumbukumbu za Uhalifu.
- (vii) Awe hajaoa au kuolewa.
- (viii) Asiwe na alama za kuchorwa mwilini (Tatoo).
- (ix) Awe hajawahi kutumia aina yoyote ya madawa ya kulevywa.
- (x) Awe tayari kuhudhuria mafunzo ya taaluma ya Zimamoto na Uokoaji.
- (xi) Awe hajawahi kuajiriwa serikalini.
- (xii) Awe mwenye urefu usiopungua futi 5.7 kwa mwanaume na futi 5.4 kwa mwanamke.
- (xiii) Awe tayari kujigharamia katika hatua zote za usaili.

## 5. Utaratibu wa Kutuma Maombi

- (i) Barua za maombi ziandikwe na mwombaji kwa mkono zikiambatishwa na nakala zifuatazo:-
- (a) Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
  - (b) Fomu ya uthibitisho wa siha njema kutoka kwa mganga wa serikali.
  - (c) Nakala ya Kitambulisho cha Taifa au namba ya NIDA.
  - (d) Nakala ya cheti cha kufuzu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)
  - (e) Picha tatu za Pasipoti.
  - (f) Nakala ya cheti cha Taaluma/ujuzi husika kinachotambulika na mamlaka za elimu nchini (Kwa wale wenye taaluma/ujuzi).
  - (g) Barua ya Utambulisho kutoka kwa afisa mtendaji wa Kijiji/mtaa au mkuu wa Kambi ya JKT kwa wale waliopo kwenye Kambi za JKT.


NB. Nakala za vyeti zithibitishwe na Kamishna wa viapo au Hakimu.

- (ii) Kwa waombaji wenye elimu ya kidato cha nne, astashahada Trade Test Grade I, na FTC waelekeze maombi yao kwa Kamishna Jenerali, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na maombi yao yatumwe kwa Kamanda wa Mkoa husika, anwani za Makamanda zimewekwa katika **Kiambatisho A**

- (iii) Kwa waombaji wenye elimu ya kidato cha sita na Shahada/Stashahada ya Juu waelekeze maombi yao moja kwa moja kwa:-

**Kamishna Jenerali,  
Jeshi la Zimamoto na Uokoaji,  
S.L.P. 1509,  
DODOMA.**

- (iv) Barua zitakazowasilishwa mkononi **hazitapokelewa.**
- (v) Waombaji wote waandike namba ya simu katika barua zao za maombi
- (vi) Mwombaji atakayewasilisha nyaraka za kughushi au taarifa za uongo atachukuliwa hatua za kisheria
- (vii) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **15 Oktoba, 2021.**

  
CF - M. S. Semwanza, ndc  
**Kny. KAMISHNA JENERALI  
JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**